*Jiwe la kiroho la kujengea No. 94*

# KWA MUDA GANI YESU KRISTO ATAKUWEPO KAMA KUHANI WETU MKUU NAMPATANISHI?

**(SehemuI)**

*"Basi iwapo tunaye kuhani mkuu aliyeingia katika mbingu, Yesu, Mwana wa MUNGU, na tuyashike sana maungamo yetu. Kwa kuwa hakuna kuhani mkuu asiyeweza kuchukuana nasi katika mambo yetu ya udhaifu; bali yeye alijaribiwa sawasawa na sisi katika mambo yote, bila kufanya dhambi. Basi na tukikaribie kiti cha neema kwa ujasiri, ili tupewe rehema, na kupata neema ya kutusaidia wakati wa mahitaji"* ( Waebrania 4:14-16).

Sikilizeni kile nabii wa Mungu akizungumzia kuhusu hilo:

Sasa, zile siri za kile Kitabu zinafunuliwa wakati Mihuri inapovunjwa. Na wakati Mihuri imevunjwa kabisa, wakati wa ukombozi umekwisha; kwa sababu Mwana-Kondoo ameondoka kwenye hema ya upatanisho, apate kwenda na kutwaa madai Yake. Yeye alikuwa Mpatanishi, kati ya hayo. Lakini wakati ufunuo halisi unapotukia juu ya Mihuri, wakati inapoanza kufunguka, Mwana-Kondoo anakuja kutoka madhabahuni. Ni kulingana na Neno. Yeye alikuja akitokea katikati, na kukitwaa kile Kitabu, kwa hiyo Yeye si Mpatanishi tena. Kwa sababu, hata walimwita Simba, na huyo ni Mfalme, wala si Mpatanishi wakati huo.

Basi, Mwana-Kondoo, katika wakati wa upatanisho *hapa* nyuma, Yeye alijua ya kwamba kulikuwako na majina ndani humo yaliyowekwa ndani humo tangu kuwekwa misingi ya dunia. Na mradi majina hayo hayajadhihirishwa duniani bado, ilimbidi Yeye kukaa hapo kama Mpatanishi. Mnaelewa? Kuchaguliwa tangu zamani, kikamilifu…..

Vema. Ilimbidi kukaa pale, kwa sababu Yeye alikuja kuwafia wale ambao Mungu aliwakusudia Uzima wa Milele(Matendo13:48). Kwa kujua Kwake tangu zamani, Yeye aliwaona. Si kwa mapenzi Yake Mwenyewe; mapenzi Yake yalikuwa kwamba hata mmoja asipotee (I Timotheo 2:3-4). Lakini kwa kujua Kwake tangu zamani Yeye aliwajua wale ambao wangepotea na wale ambao hawangepotea.

Kwa hiyo, mradi tu kulikuwa na jina moja ambalo lilikuwa bado, kamwe halijatangazwa duniani, ilimbidi Kristo kukaa hapo kama Mpatanishi,kushughulikia jina hilo. Lakini mara tu jina hilo la mwisho lilipotumbukizwa katika hiyo Kloroksi ama kitakasaji, basi siku Zake za

upatanisho zilikuwa zimekwisha. “Yeye aliye mchafu na abaki mchafu. Yeye aliye mtakatifu, angali ni mtakatifu.” (Ufunuo 22:11). Ndipo anaondoka kwenye ile madhabahu, na ndipo inakuwa ni Kiti cha Hukumu. Ole wao hao walio nje ya Kristo wakati huo.

Unaona, si Mungu, kama tunavyodhania, anayeenda kujitafutia watu elfu chache wa wakati huu na kuwatwaa. Ni wale Wateule halisi toka katika kila wakati. Na hiyo ndiyo sababu Kristo hana budi kukaa kwenye kiti cha upatanisho huku nyuma, kama Mpatanishi, mpaka yule wa mwisho aingie katika wakati wa mwisho. Na mafunuo haya basi, ya yale yaliyokwisha tukia, yatafunuliwa kwa watu, nao wanaona yaliyotukia. [1]

Sasa, na tunaona ni Kitabu cha Ukombozi. Ndipo tulirudi nyuma na tukampata yule Mkombozi aliye Jamaa wa Karibu, na tukamchukua, kuona kazi yake ilikuwa ni nini. Na sasa kwa miaka hii yote, Kristo amekuwa akifanya kazi ya Mkombozi aliye Jamaa wa Karibu. Yeye amekuwa akifanya kazi ya Mkombozi aliye wa Jamaa wa Karibu. (Walawi 25:25-28). Lakini utakuja wakati kwamba ambapo kazi ya kukomboa itakwisha. Na hapo kazi ya kukomboa itakapokwisha, basi Yeye ataondoka kwenye Kiti cha Enzi cha Mungu, mahali ambapo ameketi sasa. Lakini hicho si Kiti Chake cha Enzi. “Yeye ashindaye ataketi pamoja nami katika Kiti Changu cha Enzi, kama nilivyoshinda na kuketi katika Kiti cha Enzi cha Baba Yangu.” (Ufunuo 3:21). Hicho si Kiti Chake cha Enzi. Hicho ni cha Roho, Mungu. Kristo, yule Mwana-Kondoo, hicho si Chake. Yeye ni Mungu aliyefanyika mwili, ambaye ni Mungu yeye yule, aliyefanyika mwili. (Yohana 1:1-2,14, Wakolosai 1:14-15).

Yeye (Mwanakondoo) alikuwa kule nyuma, akifanya kazi Yake ya upatanisho; kwa sababu Yeye alikuwa akitoka damu kwa ajili ya watu, akiwaombea watu, mpaka yule mtu wa mwisho, aliyeandikwa kwenye Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo kabla ya kuwekwa misingi ya dunia, aingie (Ufunuo 5:1-5; Ufunuo 13;8-9). Kutakuwa tu na wengi wao kule, na ndio basi. Basi. Hao wengine hata hawatataka kuingia; hawana hamu ya kuingia. Na kwa hiyo, basi, wakati huyo mtu wa mwisho atakapoingia, basi wakati wa ukombozi umekwisha. Ndipo Mwana-Kondoo anakuja kudai haki Yake ya wale aliowakomboa, na hiyo ni uumbaji wote. Dunia na kila kitu ni mali Yake. Mnaona? Yeye ameikomboa kwa Damu Yake Mwenyewe. Na wakati anapokuja kukichukua Kitabu hiki, kukifungua, mbona, jamani, wao walikuwa…(ufunuo 5:1-10)Yohana hakulia tena. Ndipo akaangalia, na Mwana-Kondoo huyu alikuwa Mwana-Kondoo aliyechinjwa. Alikuwa ameuawa tayari, bali alikuwa hai tena.

Na sasa tuliona ya kwamba mwana-kondoo aliyechinjwa ni mwana-kondoo aliyelowa damu, akitoka damu kila mahali. Amechinjwa tayari. Na baada ya kuchinjwa, alifufuka tena. Alikuwa ameketi kwenye Kiti cha Enzi, tuseme, nyuma huko ya Kiti cha Enzi, namna *hii*, akiziombea nafsi zote zile ambazo zingekuja. Ndipo wakati yule wa mwisho alipofika, na ilikwisha,Mungu angali alikuwa ameshika kile Kitabu cha Ukombozi. Sasa Yeye anafanya tu kazi ya Jamaa wa Karibu,Kama vile, Boazi alivyoshuka kule, na Ruthu alikuwa tu ameketi pale akingojea mpaka Boazi…. Namaanisha Boazi alipomaliza kazi ya ukombozi wa Jamaaya karibu (Ruth 4).

Sasa ulimwengu ungali unakuwa mbaya zaidi. Na dhambi inalundikana, na magonjwa, na shida, na kifo, na huzuni. Sasa angalia. Lakini basi baada ya yote kwisha, baada ya Uombezi

Wake kwisha, Yeye anatokea, anakichukua kile Kitabu kutoka kwenye mkono Wake. Na ndipo Yohana, na kila kitu Mbinguni, na Zile roho zilizo chini ya madhababu zinaanza kupiga makelele. Na jinsi walivyofurahia! Nao wakaanguka kifudifudi, wale wazee, na kumwaga maombi ya watakatifu (ufunuo 8:1-5). Na zile roho chini ya madhababu zikapaza sauti, "Umestahili Wewe, kwa sababu umetukomboa kwa Mungu, nasi tunarudi duniani kuishi kama wafalme na makuhani." (Ufunuo5:8-10).

Ndipo Yohana akasema, "Kila mtu Mbinguni, kila kitu chini ya nchi, na kila kitu," kilimsikia akimsifu Mungu kuhusu jambo hilo. Hapana budi Yohana aliona jina lake Pale, unajua…. Wakati wote huo…(ufunuo 5:11-14).

Ndipo aliposema, "Yeye amestahili kukitwaa kile Kitabu cha Ukombozi." Sasa si mali ya yule Hakimu tena. Ni mali ya Mkombozi, Naye ameisha maliza kazi ya ukombozi.

Sasa anakwenda kulionyesha Kanisa yale aliyokwisha kufanya. Unaona? Ndipo anachukua tu…Lakini kile Kitabu kimefungwa. Hakuna mtu aliyejua, kamwe. Wao wanajua kilikuwa ni Kitabu cha Ukombozi, juu Yake pale, lakini ilibidi kifunuliwe katika siku za mwisho. Kulingana na Ufunuo 10, yule malaika wa saba atapewa Ujumbe wa Hayo. Kwa sababu, ilisema, ya kwamba, "Katika wakati wa kutangazwa kwa wakati wa saba wa kanisa, malaika wa saba, wakati atakapopiga baragumu, siri zote za Mungu zitamalizika, kwa kupiga kwake baragumu." Halafu, baada ya kufunuliwa Kwake, yule Malaika anashuka kutoka Mbinguni, ambaye alikuwa ni Kristo. Sasa kumbukeni, malaika huyu yuko duniani, mjumbe.

Kristo anashuka, (unamwona katika sura ya 10 ya Ufunuo); anaweka mguu mmoja juu ya nchi, na huo mwingine juu ya bahari; upinde wa mvua juu ya kichwa Chake, macho yake kama…na miguu kama moto, na kadhalika; anainua mkono Wake, na kuapa kwa Yeye aishiye milele na milele, kwenye Kiti cha Enzi, ya kwamba, "Hakutakuwa na wakati baada ya haya." Na hapo anapoapa kiapo hiki, Ngurumo Saba zinatoa sauti zao.

Mwana-Kondoo anaketi pale, akifanya upatanisho, mpaka wa mwisho atakapoingia. Ile kengele ndogo inalia, Naye anatoka na kuchukua mali Yake basi, hivo; analileta kanisa Lake Nyumbani, raia Wake. Ndipo tunatoka tunaingia katika ule Utawala wa Miaka Elfu (Isaya 65:17-25). [2]

Sasa, hebu uchunguze tu moyo wako, ndugu yangu, dada yangu, rafiki yangu. Mtafute Kristo sasa wakati una nafasi ya kumtafuta (Isaya 55:6-7). Huenda likatokea hivi karibuni sana ambapo huwezi kumtafuta. Anaweza aondoke kwenye kile kiti, wakati wo wote, cha upatanisho Wake; ndipo ungeweza kulia kwa moyo wako wote, ungeweza kukanyaga ardhi kwa nguvu sana, ungeweza kunena kwa lugha, ungeweza kukimbia huku na huko sakafuni, ungeweza kufanya lo lote ulilotaka, na kujiunga na kila kanisa ulimwenguni, hakuna kitu, hakuna kitakasaji tena kwa ajili ya dhambi yako. Basi uko wapi basi?

Vema, ninaamini, kwa moyo wangu wote, kile kiti kingali wazi bado. Ninaamini Yeye yungali kwenye Kiti cha Enzi cha Mungu. Lakini hivi karibuni Yeye atainuka sasa, na kujitokeza, apate kudai wale aliowakomboa. Yeye anafanya kazi ya Mkombozi aliye Jamaa wa Karibu, wakati Ruthu anangojea (Ruth 3:18).Lakini hivi karibuni, mwajua, baada ya Boazi kufanya kazi ya jamaa wa karibu, basi alikuja akadai mali yake. Na hivyo ndivyo hasa Biblia ilivyosema Yeye

alifanya, “Yeye alikuja akakitwaa kile Kitabu.” Ndipo kazi ya upatanisho imekwisha; Yeye ameondoka kwenye kile Kiti cha Enzi; hakuna Damu tena kwenye kile Kiti cha Rehema. Halafu ni kitu gani? Kiti cha Hukumu. [3]

Wakati Mwana-Kondoo alipochinjwa, majina hayo yaliwekwa kwenye kile Kitabu cha uzima cha mwanakondoo tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu (Ufunuo 13:8). Yeye anasimama katika Mahali Patakatifu usiku wa leo, Utukufuni, kama Mwombezi, akiombea kila mmoja wa watu hao ambao majina yao yako kwenye Kitabu hicho(Warumi 8:26-27; Waebrania 2:17-18). Na hakuna mtu anayejua jina hilo ila Yeye. Yeye ndiye aliyeshika kile Kitabu mkononi Mwake, Naye anajua. Wakati huyo wa mwisho atakapoingia, basi siku Zake za kuombea zimekwisha. Yeye anakuja basi kudai kile Yeye alichoombea. Yeye anafanya kazi ya Mkombozi wa Jamaa wa karibu sasa; na sasa anakuja kuwapokea Walio Wake.

Halafu akatoa hiyo Damu, kwa maana Yeye alifanyika jamaa yetu. Naye alikuwa Mkombozi aliye wa Jamaa wa Karibu (Walawi 25:25-28). Naye akamwaga hiyo Damu, kwa mapenzi Yake Mwenyewe. Haikumlazimu kufanya hivyo. Aliitoa kwa mapenzi Yake Mwenyewe, apate kukomboa. Halafu anaenda kwenye madhabahu ya Mungu, na kungojea pale, wakati Mungu amekishika Kitabu cha Ukombozi mkononi Mwake. Na yule Mwana-Kondoo aliyejaa damu anasimama kwenye ile madhabahu ya dhabihu. Huyo hapo Mwana-Kondoo, kufanya ukombozi, akituombea. [4]

Wakati sulemani alipoomba, aliomba “Bwana, watu wako watakapokua kwenye shida mahali popote na kuuangalia mlima huu mtakatifu, au mahali hapa patakatifu, na kuomba basi uwasikie kutoka mbinguni” (I Wafalme 8:22-30; 9:1-3). Na Yona alikua na ujasiri kua Mungu aliyasikia maombi ya Sulemani maana alikua mtumishi wa Mungu (Yona 2:5). Na kama angeweza kua na kiasi hicho cha matumaini kwenye ombi la mtu aliyekua akiweka wakfu hekalu la duniani, na mtu akiomba ombi hilo ambaye hatima ya maisha yake alirudi nyuma, na chini ya hali hizo, akiwana dalili za aina hiyo, angewezakua na tumaini kubwa kama hilo kwamba Mungu angesikia maombi yake, ni zaidi sana vipi sisi tunapaswa,ambao tumeketi katika uwepo wa Yesu Kristo aliyefufuka, akiangalia mbali dalili zetu kutoka mbinguni ambapo Yesu Kristo ameketi mkono wa Kuume wa Mungu (matendo 7:54-56; warumi 8:34), kwa damu yake mwenyewe akifanya maombezi juu ya maungamo yetu.

Ninaamini sasa uwepo wake uko hapa, kuniweka huru kutoka katika kila kifungo ambacho shetani ameweka juu yangu.  Na ninaangalia alipoketi katika mkono wa kuume wa Mungu, Yuhai milele akifanya upatanisho kwangu kwa Damu Yake mwenyewe. Kama kuhani mkuu ameketi pale, na ni kiasi gani tunapaswa kuangalia kwenye mahali patakatifu pa Mungu, ambapo Yesu mwenyewe, Mpatanishi wetu, pekee kati ya Mungu na mwanadamu, akisimama na Damu yake mwenyewe akifanya maombezi juu ya Maungamo yetu. Amina. “Amina” humaanisha “ Iwe hivyo”  Ninaliamini hilo kwa moyo wangu wote (Waebrania 3:1-6)

Sasa,Yesu Yule Yule ni kuhani mkuu leo. Biblia imesema hivyo (Waebrania 4:14-16). Hiyo ni sawa ndugu Wahudumu? Yule, “ Sasa ni kuhani mkuu akiketi mkono wa kuume wa Mungu,

Baba, akikaa pale aishiye milele akifanya upatanisho, Kuhani mkuu ambaye anaweza kuguswa na madhaifu yetu" Wewe sema tu Mungu, " Baba wa mbinguni, Ninaumwa. Ninahitaji msaada. Na ninatumia Imani yoote niliyonayo . Na ninaamini kwamba u Kuhani mkuu sasa. Hebu ni kuguse Bwana,na Wewe utakua yuleyule Jana…." [5]

Biblia inasema, Yeye alipaa juu, akiketi mkono wa kuume wa Mungu (Waefeso 1:20-23). Mnaamini hilo? Yeye yuko pale kufanya upatanisho, na Yeye ni kuhani Mkuu ambaye anaguswa na madhaifu yetu. Mnaamini hilo? Mpatanishi wetu pekee kati ya Mungu na Mwanadamu ni Yesu Kristo. Hiyo ni kulingana na Biblia (I Timotheo 2:5-6). Mnaweza kua na wengine wakijaribu hilo. Lakini kunaye mmoja pekee ambaye Mungu humsikia, na huyo ni Yesu Kristo. Hiyo ni sawa. Angalia, jinsi tu vile ameketi pale kama kuhani Mkuu, Yeye Yule Jana, Leo na hata milele.

Sasa kama yeye aangelikua akitembea hapa, na unaimani kwamba angelikuponya,.. Sasa, Mwamini Mungu katika Neno lake, wewe mwamini Mungu ndani ya watu wake.

Yesu alifufuka toka katika wafu, akarudi katika Roho Mtakatifu,na kurudi tena kuishi ndani ya watu wake kufanya kazi zilezile alizokua akizifanya. Na saa imekaribia ya haya kutimizwa, ' sababu mwisho wa wakati wa Mataifa upo karibu. Yeye alifanya hilo katika mwisho wa Uyahudi, mwisho wa usamaria, na sasa mwisho wa mataifa, kama tu vile alivyofanya basi: ameahidiwa kufanya hilo kulingana na maandiko. [6]

Sasa, Yeye ni kuhani mkuu wa maungamo yako, Yeye anaweza tu,kukusaidia wewe kwa kadri utakavyoliamini hilo. Kama umetubu dhambi zako, kama umetubu makosa yako, kama umemaliza kila kitu, Umekiri umekua asiyejali, chochote ulichoungama, sasa kinawekwa juu ya madhabahu ya dhabihu. Sasa, weka mkono wako juu ya Yesu na ujitambulishe mwenyewe. Unajitambulisha kwa Imani.Weka mikono yako juu ya Yesu. Na unapofanya hivyo,angaliia kwake na useme, " Ninapokea hilo Bwana,Ninakuamini wewe sasa"

Oh, unaliamini hilo sasa, na dhabihu yako kwenye madhabahu… Juu ya madhabahu,umeweka nini pale, tofauti zote, umeziweka madhabahuni, sasa kwa Imani, weka mikono yako juu ya dhabihu yako, Yesu, Ambaye ameketi mkono wa Mungu kufanya upatanisho kwaajili yako kuhusu maungamo yako kwamba unaamini kwa moyo wako wote kua atapokea kile ulichotoa kwake. ( Waebrania 7:25-27). Kama utaamini kwamba Yesu Kristo amepokea kile ulichomtolea asubuhi hii, " Ninakupa maisha yangu Bwana. Nimekua wa baridi; Nimekua asiyejali. Nimefanya mambo sikupaswa kufanya. Lakini kuanzia saa hii,nahitaji kusogea juu karibu na wewe, na ninaamini kwamba nitapokea hilo. Ninaweka mikono yangu juu yako sasa ninapofanya maungamo yangu" [7]

Wakati alipokuwa hapa duniani, kama ninavyosema, Yeye aliwajali watu sana hata akawaponya wagonjwa wao, akaifariji mioyo yao, akawaambia kuhusu ma—mahali ambapo Yeye angeenda na kuwaandalia, kisha arudi tena kuwapokea Kwake. Aliwajali. Na hebu angalia, Yeye alijali sana mpaka, wakati alipojua ya kwamba hana budi kuondoka kusudi atuletee kitu hiki kikubwa, Yeye alisema, "Sitawaacha ukiwa, bali nitamtuma Roho Mtakatifu, Naye ataendeleza fadhili Zangu kwenu," mpaka Yeye atakaporudi (Yohana 14:15-20). Hakuna mtu

anayejali kama Yesu. Tukijua ya kwamba mwili Wake, kama Kuhani Mkuu, katika kazi ya uombezi anayofanya sasa, Mwili huo hauna budi kuwa Mbele za Mungu wakati wote, kwa ajili ya uombezi, ili kwamba Mungu asiweze kuiona dhambi ya mwenye dhambi; Yeye anaona tu Damu ya Mwanawe. Na tukijua ya kwamba, Yeye alimtuma Roho Mtakatifu arudi aendelee kuwafariji watu Wake. Je! Yeye anajali? Hakika, Yeye anajali. Sasa, alikuwa aendelee kuwajali watu Wake, watu Wake hapa duniani, kwa jinsi ile ile aliyowajali wakati alipokuwa hapa.

Mtu mmoja alianguka akafa papa hapa jukwaani, papa hapa mbele zetu, karibu majuma matatu yaliyopita. Mkewe ni nesi aliyesajiliwa Alimchunguza, hamna moyo, hamna pigo. Nikaweka mikono yangu juu yake (alikuwa ameaga) nami nikaiita tu roho yake, katika Jina la Yesu Kristo, naye akafufuka. Unaona? Unaona?Ni kitu gani? Yeye Ndiye ufufuo na Uzima (Yohana 11:25-25). Haikuwa ni mimi. Huyo aliyetenda kazi ni Mfariji, Roho Mtakatifu akituombea. Mnaona? Tumemkubali, sasa ni juu Yake kutuombea. Je! Mungu angeweza kukuokoa kinyume cha mapenzi yako? La hasha. Hawezi kukuokoa kinyume cha mapenzi yako. Huna budi kuamini.

Biblia ilisema ya kwamba Yeye ni Kuhani Mkuu, sasa hivi Kuhani Mkuu, ameketi mkono wa kulia wa Ukuu wa Mungu, kutuombea tunapokiri. Tunaungama tunamwamini, nasi tunataka kumgusa Kuhani mkuu. Nasi tukimgusa, Yeye angefanya nini? Yeye yupo hapa katika umbo la Roho Mtakatifu. Ndipo angeweza kujibu moja kwa moja na kukwambia vile vile hasa. Hiyo ni kweli? [8]

Lakini kwenye ile Muhuri ya Sita, mahali ambapo Baragumu hizi zilifunguliwa…(Ufunuo 6:12-17). Kumbukeni, kwenye huo, tunaona ya kwamba Mwana-Kondoo alikuja, akajitokeza hadharani. Yeye alikuwa ameondoka kwenye Kiti cha Rehema. Kazi Yake ya Ukombozi ilikuwa imekwisha. Ndipo akaja akakitwaa kile Kitabu kwenye mkono wa kuume wa Yeye aliyeketi kwenye Kiti cha Enzi, na "hakukuwa na wakati baada ya hayo." Ndipo mara moja malaika akatokea katika sura ya 10 na aya ya 7, Malaika huyu alishuka akaapa, kwamba, "hapana wakati tena." Lakini, mnaona, ndani ya Kitabu hiki mlikuwemo na kile kilichokombolewa. Kilikuwa ni Kitabu cha Ukombozi. Na kila kitu alichokuwa amekomboa kilikuwa kimeandikwa katika Kitabu hicho. Na yote aliyofia yalikuwa yameandikwa katika kile Kitabu, wala Yeye hangeweza kuondoka kwenye Kiti Chake cha maombezi mpaka Yeye amekomboa kabisa. Wala Yeye asingeweza kukikomboa pale msalabani, kwa maana wao walichaguliwa tangu awali katika Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo, naye ilimbidi kukaa Mle kufanya maombezi hata mtu yule wa mwisho amekwisha. Utukufu! Lakini siku moja akainuka kutoka Kule, akaja. Kile Kitabu kilikuwa wapi? Kilikuwa bado kiko kwa Mwenyewe asiyeonekana, Mwenyezi Mungu.

Wakati hizi Muhuri Saba zilipofunguliwa, hilo lilifungua Biblia nzima. Zile Muhuri Saba; kilikuwa kimetiwa muhuri kwa Siri Saba, na katika hizi Muhuri Saba kulikuwemo na siri Yake yote. Nacho kilikuwa Kitabu cha Ukombozi, Agano Jipya.Si la Kale. Lilitangaza tu Agano Jipya. "Wao hawawezi kukamilishwa pasipo sisi," (Waebrania 11:39-40). Mnaona? Naam, ukombozi ulikuja tu wakati yule Mkombozi alipokufa. Nao walikuwa kwa uwezekano chini ya damu ya wana-kondoo, si Mkombozi; wao hawakuwa wamekombolewa bado, mpaka yule Mkombozi alipokuja.Yohana akaangalia kila mahali, wala hapakuwepo na mtu Mbinguni, wala

mtu duniani, hamna mtu, hakuna Malaika, hakuna kitu kingaliweza kukichukua kile Kitabu wala kuzifungua zile Muhuri, wala hata kukitazama. Hakuna mtu aliyestahili. Yohana alisema alilia kwa uchungu, sababu hakukua na mtu hata astahiliye kukitazama Kitabu. Na ilibidi kufungua mihuri kufunua kile kilichokua zile siri. Siri zilikua ndani ya mihuri saba.Ndipo Malaika akamjia, kasema, "Usilie, Yohana, kwa maana Simba wa kabila la Yuda ameshinda, Naye anastahili."(Ufunuo 5:1-10)

Ndipo Yohana akaangalia apate kumwona simba, naye aliona kitu gani? Mwana-Kondoo, naye alikuwa Mwana-Kondoo aliyejaa Damu, Mwana-Kondoo aliyekuwa amechinjwa( I Petro 1:18-20). Kwa muda gani? Tangu kuwekwa misingi ya dunia.(Ufunuo13:8) Mwana-Kondoo akaja, akaenda moja kwa moja kwa yule aliyekuwa na kile Kitabu katika mkono Wake wa kuume, akakipokea kile Kitabu; akapanda kwenye Kiti cha Enzi akaketi. Haya basi. Ilikuwa imekwisha (lini?) wakati zile Muhuri zilipofunuliwa. Wakati yule wa mwisho.., hayo yalikuwa ndiyo kila kitu alichokuwa amekomboa, hapakuwepo na kitu…Alikuja kukomboa.

Kasema, "Kwa nini Yeye hakuwakomboa miaka arobaini iliyokwisha? Miaka elfu mbili iliyokwisha?" Mnaona, majina yao yako kwenye Kitabu cha Uzima, kwenye hicho Kitabu. Naye ilimbidi kusimama hapa, kwa maana ilikuwa ni kusudi la Mungu kuwakomboa. Majina yao yaliandikwa kwenye Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu. Mwana-Kondoo aliwekwa kule pamoja nacho, apate kuuawa. Huyu hapa Mwana-Kondoo anakuja, alipochinjwa, akirudi kufanya maombezi.

Mwangalie! Kutakuwa na kuiga kwingi sana, wingi wa cho chote kile, bali kulikuwa hasa na mtu ambaye angeokolewa, kwa kuwa Kanisa lilichaguliwa tangu awali kuwa…. lisilo na waa wala kunyanzi. Litakuwepo (Waefeso 5:25-27). Naye Mwana-Kondoo alikufa kwa ajili hiyo. Halafu tena wakati lile jina la mwisho katika kile Kitabu lilipokombolewa, Mwana-Kondoo alitokea akakichukua kile Kitabu, "Mimi Ndimi niliyefanya jambo hili!" [9]

Unaona, wote katika wakati wa Luther, Yeye aliwatoa. Wote katika wakati wa Wesley, Yeye aliwatoa. Wote katika nyakati mbalimbali, na wakati wa Upentekoste, Yeye aliwatoa. Wako upande huu, hawatahukumiwa pamoja nao. Watanyakuliwa. Na basi wakati jina la mwisho litakapotokea, ambalo liliwekwa kwenye Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo, ambaye alichinjwa kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu; wakati jina la mwisho limekwisha kukombolewa, kazi Yake imekwisha. Yeye anajitokeza kuja kudai ambacho Yeye amekikomboa. Hilo hufanya mioyo yetu ione huruma nyingi. Lakini kama ingeendelea miaka elfu moja baadaye, kusingekuwepo na mmoja atakayekombolewa.Na hakuna mtu anayeweza kukombolewa isipokuwa waliandikwa kwenye Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo kabla ya kuwekwa misingi ya dunia. Ni akina nani? Sijui. Hakuna mwingine ye yote ajuaye, unaona, ni Mungu peke yake. Natumaini kwamba kila mmoja wetu, majina yetu yako kwenye Kitabu kile. Kama langu lilikuwepo mle, nina hakika nitakuwa kule; kama halikuwepo, sitakuwepo kule. Ni hivyo tu. Unaona, hiyo ni kazi ya Mungu tu. "Si katika uwezo wake yeye atakaye, wala wa yeye apigaye mbio, bali Mungu arehemuye." (Warumi 9:14-16). [10]

<u>Nukuu:</u>

[1] "Muhuri wa kwanza" (63-0318), aya 51,59-60,105
[2] "Muhuri wa tatu" (63-0320), par. 29, 34-35, 37-42, 272
[3] "Muhuri wa nne" (63-0321), par. 393- 394
[4] "Muhuri wa sita" (63-0323), par. 63, 134

[5] “Aliyemkuu kuliko Suleimani Yuko hapa” (63-0605), par. E-43-E44 + E-91
[6] “Tuonyeshe Baba” (63-0606), par. E-98
[7] “Makongamano” (63-0608), par. E-114-E-115
[8] “Yeye hujali, Je wewe unajali?”, (63-0721), par. 34, 173-174, 177
[9] “Nafsi zilizoko kifungoni sasa” (63-1110M), pg. 24-25
[10] “Yeye aliyendani yenu” (63-1110E), par. 45

---

Jiwe la kiroho la kujengea na. 10 kutoka kwenye Neno lililofunuliwa la saa hii, Yamekusanywa na Gerd Rodewald friedenstr. 69 D-75328 Schomberg, Germany Simu (+49) 72357613 Fax: (+49) 72353306

---

Anakuja mmoja na ujumbe ambao ni moja kwa moja ni Biblia na kazi ya haraka itazunguka dunia. Na mbegu zitaingia magazetini, vitu vya kusomea, mpaka kila mbegu iliyokusudiwa kimbele imesikia.

(Ndugu Branham katika mwenendo utaratibu na mafundisho uk 724)

*Kwa nakala zaidi za kiingereza au kiswahili Andika kwa:*

*Joseph C Kanju*
*Box 553 Korogwe - Tanga*
*E-mail: kanjujoseph23@gmail.com*
*Cellphone: 0654335361*